KARIBUNI TENA KATIKA KUYATAFAKARI MAANDIKO YA MUNGU WETU
"INAWEZEKANA KUISHI MILELE"
SOMO LA TATU LINASEMA: **Kuna Kanuni Gani Rahisi Za Kuishi Milele?**

Fungu Kuu: *"Na uzima wa milele ndio huu wa kujue wewe, MUNGU wa pekee wa kweli, na YESU Kristo uliye mtuma"* **Yohana 17:3**

Na. Dkt. Edward Raphael Mhina

Ndugu msomaji katika mambo ambayo wengi wanapotea au kupoteza fursa ya kuishi milele ni kwa kukosa kujua ukweli kutoka ndani ya biblia. Miongoni mwa kweli hizo ni pamoja na kanuni rahisi ambazo MUNGU kwa mkono wake aliziandika na kumpatia mwanadamu ili kwa kumwamini Yesu aishi milele. Ukisoma katika kitabu cha **Kutoka 31:18** ***"Hapo Bwana alipokuwa amekwisha zungumza na Musa katika mlima wa Sinai, akampa hizo mbao mbili za ushuhuda, mbao mbili za mawe, ZILIZOANDIKWA KWA CHANDA(KIDOLE) CHA MUNGU".*** Hivi tunaona ya kwamba ni za muhimu kiasi gani kuzifuata sababu MUNGU ameziandika kwa mkono wake mwenyewe. Hii ni kuonyesha ya kwamba atuwezi ishi maisha ya amani bila kuzifuata amri hizi katika ulimwengu huu ambao shetani anafanya kila njia, ili tusifanye yale MUNGU anayotuagiza kuya tenda. Kanuni hizi ni nyepesi kuzifuata ikiwa tutajikabidhi kwa Yesu kwamba atusaidie maana biblia inasema si nzito, ukisoma **1 Yohana 5:3**, ***"Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito."*** Ili mtu azishike kanuni za Mungu kwa ukamilifu wake anahitaji msaada wa Yesu na Roho mtakatifu atukamilishae katika mambo yote, ***"Nayaweza mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu"***

Paulo katika kitabu cha **Warumi 7:12** anasemakanuni hizi ni takatifu na haki tena ni njema : ***"Basi torati ni takatifu , na ILE AMRI NI TAKATIFU, NA YA HAKI, NA NJEMA".*** Hata ukitazama vitu vyote vinavyo tengenezwa vina vijitabu vinavyo beba maelekezo ya namna ya kuvitumia ili vidumu kwa muda mrefu bila matatizo. Vivyo hivyo kwa mwanadamu ili aweze kuishi maisha yamilele akimpendeza yule aliye muumba hana budi kuishi kulingana na amri kumi za MUNGU kanuni rahisi za upendo za kuishi milele. Kanuni hizo huonesha tabia ya Mungu kwa mwanadamu kuwa ni ya upendo, ukamilifu, utakatifu na njema.

Ukweli ni kwamba kuna amri kumi za MUNGU ambazo ni kanuni za upendo nazo zinapatikana katika kitabu cha kutoka 20:1-17na kimsingi amri hizi zimegawanyika katika makundi mawili kama vile YESU alivyo jibu katika kitabu cha Mathayo22:36-40 pale alipo ulizwa swali ***"Mwalimu, katika torati ni amri ipi iliyo kuu? 37 Akawaambia, Mpende Bwana MUNGU wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote.38 Hii ndio amri iliy kuu tena ya kwanza, 39. Nayapili yafanana nayo, nayo ni hii, Mpende jirani yakokama nafsi yako .40. Katika amri hizi mbili hutegemea torai yote na manabii"***

© ShareHope Ministries 2015

Ndugu msomaji ukiangalia kwa umakini YESU alikuwa akimaanisha ya kwamba kutoka kanuni/amri ya kwanza mpaka ya nne huonesha mahusiano ya upendo yaliyopo katiya MUNGU na mwanadamu na kuanzia kanuni/amri ya tano mpaka kumi huonesha mahusiano ya upendo kati ya wanadamu. Ukweli ni kwamba tukitaka kumpenda YESU nilazima tuzishike amri zake yeye mwenyewe anasema katika, **Yohana 14:15** ***"Mkinipenda, mtazishika amri zangu."***

Tahadhari ni kwamba twapaswa kuzishika amri zote kama yeye mwenyewe alivyozitoa hatuna mamlaka yakubadili wala kuiacha moja wapo **Yakobo 2: 10** anatuambia ya kwamba ***"Maana mtu awaye yote atakayeishika sheria yote, ila akajikwaa katika neno moja , amekosa juu ya yote."*** Hakika nakuambia ya kwamba MUNGU amesema kitabu hiki ni kitakatifu kwa sababu amekindika yeye mwenyewe kupitia mitume na manabii kwa njia ya Roho Mtakatifu hivyo si kwa mawazo ya binadamu, hivyo mtu yoyote atakaye jaribu kuondoa hata neno katika kitabu hiki naye ametoa onyo katika kitabu cha **Ufunuo 22:18-19** ***"Namshudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mtu yeyote akiyaongeza,MUNGU atamuongezea hayo mapigo yaliyo andikwa katika kitabu hiki,19 Na mtu yeyote akiondoa lolote katika maneno ya unabii wakitabu hiki,MUNGU atamuondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima , na katika ule mji matakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki"***

Napendekeza kwako ya kwamba tuifuate ile amri ambayo MUNGU wetu wa mbinguni kwa mkono wake alituandikia na wala si zile ziliowekwa na wanadamu maana hii ndiyo jumla itupasayo ili tuwe katika maisha ya uzima kwa kumwamini Yesu mwenye kuanzisha na kuhitimisha imani yetu. **Mhubiri 12:13**, ***"Hii ndiyo jumla ya maneno; yote yamekwisha sikiwa; Mche Mungu, nawe UZISHIKE AMRI ZAKE, MAANA KWA JUMLA NDIYO IMPASAYO MTU."***

Yapo mafungu mengi katika biblia yanayothibisha haya yote tuliyo yasoma.
"USIDANGANYIKE." Ninakualika kuuliza swali lolote linalo kutatiza uli upate majibu yaliyo sahihi kupitia kitabu cha MUNGU yani BIBLIA.

Sali nami sala hii tunapo hitimisha somo hili:

MUNGU unayetupenda sana na unayetamani tuishi kulingana na amri zako kanuni rahisi za kuishi milele na takatifu, fungua akili zetu ili tukupende wewe BWANA na kwa kufanya hivyo tukizishika amri zako kwa kuwezeshwa na Yesu pamoja na Roho wako Mtakatifu, nisaidie nisikose kujifunza neno lako tena, nimeomba kwa jina la YESU KRISTO amen!

KARIBUNI TENA TUTAENDELEA KUTAFAKARI NENO LA MUNGU WETU.

SOMO LINALOFUATA: **Je, Ninawezaje Kupata Pumziko la Milele?**

Maswali, Maoni au Ushauri wasiliana nami: **+255652648737** au **+255768678122**

© ShareHope Ministries 2015